AAMRIWA kurudisha hati hii mnamo au kabla ya tarehe......................
............Mwaka...................... Pamoja na maelekezo ya namna ulivyotekeleza hiyo.

...wa na mimi na kugongwa muhuri wa Mahakama leo tarehe..........................mwezi
............ Mwaka..................

Muhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi umebandikwa katika Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio la Kikao cha Baraza la Madiwani ...kilichofanyika na kufanyika tarehe 19 mwezi 9 mwaka 2007 mbele ya ...wafuatao:

L.S.

BIBI KUDRA J. MWINYIMVUA,
*Mkurugenzi Mtendaji,*
*Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi*

MHE. SALIM M. KIBONGE,
*Mwenyekiti,*
*Halmashauri ya wilaya ya Kilindi*

NAKUBALI

Dodoma,
18 Mei, 2009

MHE. MIZENGO KAYANZA PETER PINDA (MB.),
*Waziri Mkuu*

---

TANGAZO LA SERIKALI NA. 251 la tarehe 24/7/2009

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*Zimetungwa chini ya kifungu cha 7 na 13*

SHERIA NDOGO ZA (KODI YA HUDUMA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA KILINDI, 2009

## SEHEMU YA KWANZA

### MASHARTI YA MWANZO

1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (Kodi ya Huduma) za Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi,2009 na zitaanza kutumika mara baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali. Jina na tarehe ya kuanza kutumika

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi. Matumizi

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa kama itaelezwa vinginevyo;- Tafsiri

"Sheria" maana yake ni sheria ya fedha za Serikali za Mitaa;

"Afisa Muidhiniwa" maana yake ni mtu ye yote ambaye ameajiriwa, ambaye yumo katika utumishi wa Serikali za Mitaa na amba ameidhiniwa na Mkurugenzi kutekeleza jukumu lo lote chini ya Sher Ndogo hizi;

"Kodi" maana yake ni kodi ya huduma;

"Mlipa kodi" maana yake itajumuisha Kampuni au Shirika la kibiash ikiwa ni pamoja na matawi ya shirika hilo yanayojihusisha na shugh za kiuchumi katika eneo la mamlaka ya Halmashauri, amba yamesajiliwa;

"Mawasilisho" maana yake ni mawasiliano yote ya kodi, nyaraka maelezo yo yote yanayohitajika kuwasilishwa kwa Halmashauri kutok kwa mlipa kodi;

"Mwaka wa fedha" maana yake ni mwaka wa fedha kwa mujibu w kalenda ya mwaka wa fedha kama itakavyotambuliwa na Serikali;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, itajumuisha mtu ye yote aliyeteuliwa kufanya kazi za Mkurugenzi;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi;

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa

## SEHEMU YA PILI

### JINSI YA KUTOZA KODI

Kodi Sheria Na. 15 ya mwaka 2003

4.–(1) Halmashauri itatoza kodi itakayojulikana kama kodi ya hudum na itatozwa kwa kiwango cha asilimia 0.3% ya mauzo ghafi ya kila mwez baada ya kuondoa kodi ya ongezeko la Thamani (VAT) na ushuru w bidhaa kutokana na shughuli zote za kiuchumi zinazofanywa na mlip kodi katika eneo la mamlaka ya Halmashauri.

(2) Kodi itatozwa na Halmashauri kutoka kwa mlipa kodi ye yot anayejihusisha na shughuli za kiuchumi katika eneo la Halmashauri.

Wakala

5.–(1) Halmashauri inaweza kutangaza zabuni ya ukusanyaji wa kodi ya Huduma kama itaonekana inafaa, na kumteua wakala ikiwa ni Mtu binafsi au Kampuni, Asasi au Taasisi, ambaye ataingia mkataba wa uwakala na Halmashauri ili kukusanya kodi ya huduma.

(2) Wakala atakayeteuliwa na Halmashauri kutekeleza jukumu lo lote chini ya Sheria Ndogo hizi, atawajibika kusimamia ukusanyaji huo kwa viwango vilivyobainishwa chini ya Sheria Ndogo hizi.

(3) Wakala atakayeteuliwa kama wakala chini ya Sheria Ndogo hizi, atakuwa na majukumu ya kukusanya kodi na kumshtaki mtu ye yote atakayeshindwa kwa makusudi kulipa kodi anayotakiwa kulipa kwa wakala huyo kwa muda unaotakiwa katika mahakama yenye mamlaka ya kusikiliza shauri hilo.





(4) Wakala atakuwa na majukumu yafuatayo kwa Halmashauri:-

(a) kukusanya na kupokea kodi kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa kiwango kilichoainishwa chini ya Sheria Ndogo hizi;

(b) kuwasilisha mapato yote anayowajibika kukusanya kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala;

(c) kumchukulia hatua za kisheria mtu ye yote ambaye atakiuka masharti ya Sheria Ndogo hizi;

(5) Itakuwa ni kosa kwa wakala ye yote aliyeteuliwa chini ya Sheria Ndogo hizi:-

(d) kushindwa kuwasilisha fedha kwa kiwango kilichoainishwa katika mkataba wa uwakala;

(e) akiwa anafahamu kiwango kinachostahili kutozwa kutoka kwa mlipa kodi na kwa makusudi akakusanya zaidi au pungufu ya kiwango husika; na

(f) kwa makusudi akishindwa kutekeleza jambo lo lote analowajibika kulitekeleza kitendo ambacho kitaathiri mapato ya Halmashauri.

Muda na mahali pa kulipia ushuru

6.–(1) Malipo yote ya kodi yatafanywa kwa mwaka mara mbili na kila mlipaji anapolipa kodi ya ongezeko la thamani atatakiwa kulipa kodi ya ushuru wa huduma.

(2) Isipokuwa kama imelipwa kupitia kwa wakala, kodi italipwa katika ofisi za Mweka Hazina wa Halmashauri kwa njia ya ama hundi au fedha taslim.

(3) Endapo mlipa kodi, bila sababu za msingi atachelewesha malipo hayo kinyume na utaratibu uliobainishwa katika Sheria Ndogo ya 6(2) hapo juu atawajibika kuwasilisha kodi aliyostahili na riba ya 2% kwa kila mwezi wa uchelewaji.

Vielelezo

7.–(1) Malipo yote ya kodi yataambatanishwa na vielelezo vya biashara ya mlipa kodi vinavyoonyesha hesabu halisi ya jumla ya mauzo ghafi pamoja na kiasi cha malipo ya kodi anayolipa ilivyopatikana.

(2) Kabla Afisa muidhiniwa hajapokea malipo ya kodi, atapitia viambatanisho vya biashara au shughuli husika ya kiuchumi ya mlipa kodi ili aweze kujiridhisha na kuthibitisha kiasi cha kodi ilivyopatikana.

(3) Endapo Afisa muidhiniwa amepita na kuchunguza vielelezo vya mlipa kodi na akagundua udanganyifu wo wote katika vielelezo hivyo,

atavipuuza, na kadri ya uelewa wake atalinganisha kiasi cha mauzo g na kupiga hesabu ya kiasi cha kodi kutokana na mauzo ghafi hay mauzo ghafi ambayo mlipa kodi atawajibika kulipa na mlipa atawajibika kulipa kodi hiyo kutokana na hesabu hizo za Afisa muidhini

(4) Pale ambapo mlipa kodi atashindwa kuwasilisha viambata Afisa muidhiniwa atakisia kiasi cha kodi anachoona kinafaa.

(5) Ambacho mlipa kodi husika atawajibika kulipa katika m usiopungua siku ishirini na moja (21).

(6) Kodi itakayotokana na makisio ya hesabu za kodi yatakayofan na Afisa muidhiniwa chini ya Sheria Ndogo ya 7(3) na 7(4) hapo itahesabika kuwa ni kodi halali kulipwa kisheria.

Uwezo wa kudai taarifa

8.–(1) Bila ya kuathiri Sheria Ndogo ya 7 hapo juu, Mkurugenz Afisa ye yote aliyeidhiniwa na Mkurugenzi anaweza kudai taarif yote kutoka kwa mlipa kodi kumtaka mlipa kodi katika muda wa s ishirini na moja ampatie taarifa ya uzalishaji mauzo au taarifa yo yot kibiashara ikiwa ni pamoja na vipimo halisi, uwingi wa bidhaa, pamoj huduma zilizotolewa kwa thamani ya fedha katika eneo la mamlak Halmashauri.

(2) Mkurugenzi au Afisa muidhiniwa anaweza kutoa taarifa maandishi kwa mlipa kodi ye yote au wakala ye yote wa mlipa k ikimtaka mlipa kodi huyo, shirika au kampuni hiyo yenye taarifa au maele yanayohitajika kumpatia maelezo hayo katika kipindi cha siku kumi nne kutoka tarehe ya kupokelewa kwa notisi hiyo.

(3) Halmashauri inaweza kuomba taarifa ya mapato ya mlipa k kutoka kwa Tawi la Mamlaka ya Mapato Tanzania lililopo katika ene mamlaka ya Halmashauri.

Wajibu wa Kutoa taarifa

9.–(1) Mtu ye yote ambaye anawajibika kutoa taarifa kuhusiana malipo ya kodi anawajibika kutoa taarifa hizo kwa Halmashauri, mkusan kodi au wakala.

(2) Kwa madhumuni ya kupata taarifa chini ya Sheria Ndogo ya 8( hapo juu, Halmashauri, mkusanya ushuru au wakala kutegemeana na y





yote anayehusika na utoaji wa wito huo, inaweza kumuita mtu ye yote kufikia mbele yake katika muda na mahali ambapo pametajwa katika barua ya wito.

Uwezo kuingi kukagu eneo l biasha ya mli kodi

10. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kumuagiza Afisa Muidhiniwa kuingia katika eneo la biashara ya mlipa kodi ye yote na kuchunguza, kukagua na kupeleleza kumbukumbu mbalimbali za kibiashara kwa lengo la kuhakiki kodi inayolipwa.

## SEHEMU YA TATU

### MAKOSA, ADHABU NA JINSI YA KUCHUKUA HATUA ZA KISHERIA

Deni

11.–(1) Kodi au faini yo yote ambayo Halmashauri inadai kutoka kwa mlipa kodi ye yote, itakuwa ni deni la Halmashauri na litalipwa kupitia kwa Mkurugenzi au Afisa ye yote aliyeidhiniwa chini ya Sheria Ndogo hizi kwa niaba ya Mkurugenzi.

(2) Bila ya kuathiri maelezo ya jumla ya Sheria Ndogo ya 13(1) hapo juu, kuhusiana na jinsi ya kudai deni lo lote la Halmashauri Afisa ye yote aliyeidhiniwa na Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufungua shauri katika Mahakama yenye mamlaka ya kusikiliza shauri hilo na ataandaa hati ya malalamiko ambayo itaelezea uzito wa kosa na maombi.

Uwezo Mkuru genzi kumlip Mdaiw

12. Bila ya kuathiri maelezo ya jumla ya Sheria Ndogo ya 11(1) hapo juu, Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu ye yote anayedaiwa na Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hizi ikiwa mdaiwa huyo amekiri kwa maandishi kuwa atalipa deni analodaiwa pamoja na faini na kisha atapatiwa Stakabadhi ya malipo hayo.

Mdaiw anapos ndwa kulipa deni

13. Ikiwa mdaiwa ye yote atatozwa faini chini ya sheria ya 14 hapo juu na akashindwa kulipa deni hilo kwa wakati Mahakama itaendelea kusikiliza shauri hilo kama inavyosikiliza mashauri mengine na itatumia mamlaka yake ambapo ama itatoza faini isiyozidi shilingi 300,000/= au itatoa adhabu ya kifungo kwa mdaiwa ye yote kwa muda usiopungua miezi sita au vyote viwili kwa pamoja.

Kukata kutoa taarifa

14.–(1) Mtu ye yote ambaye atatakiwa kutoa taarifa chini ya Sheria Ndogo hizi, kwa makusudi akitoa taarifa ya uongo au kujaribu kutoa taarifa

ya uongo kwa Halmashauri, wakala au mlipa kodi juu ya suala lo lote linalohusiana na ukusanyaji kodi, atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia ataadhibiwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo ya 14(1) hapo juu.

(2) Mtu ye yote ambaye ametakiwa kutoa taarifa chini ya Sheria Ndogo ya 9 ya Sheria Ndogo hizi, na kwa makusudi amedharau, amekataa, au bila ya sababu za msingi ameshindwa kutoa taarifa zinazotakiwa atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini ya elfu hamsini (50,000/=) au kifungo cha miezi mitatu au vyote viwili kwa pamoja.

(3) Mtu ye yote ambaye ametakiwa kufika mbele ya Halmashauri, mkusanya kodi au wakala ili kutoa maelezo kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, asipofanya hivyo atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini ya shilingi elfu hamsini (50,000/=) au kifungo cha miezi mitatu au vyote viwili kwa pamoja.

Kukusanya ushuru bila ruhusa

15. Mtu ye yote ambaye:

(a) hajaruhusiwa na Halmashauri kwa maandishi kukusanya kodi inayokusanywa chini ya Sheria Ndogo hizi;

(b) amekusanya au amejaribu kukusanya kodi kwa kiwango ambacho hakijatajwa chini ya Sheria Ndogo hizi:
Atakuwa ametenda kosa chini ya Sheria Ndogo hizi na akipatikana na hatia ya kufanya kosa hilo, atalipa faini ya shilingi laki tatu (300,000/=) au kifungo cha miezi sita au vyote viwili kwa pamoja.

Hatua za Kisheria

16.-(1) Mashauri yote kuhusiana na malipo ya kodi chini ya Sheria Ndogo hizi, bila kuathiri haki ya mtu ye yote au mamlaka nyingine ya kufungua shauri la jinai, yatafunguliwa na Halmashauri au wakala kuhusiana na makusanyo ya kodi mbele ya Mahakama yo yote yenye mamlaka ya kusikiliza shauri hilo.

(2) Pale ambapo Halmashauri itaona inafaa kufungua shauri la madai kutokana na madai ya kodi, itafungua shauri hilo kwa mwenendo mkato (summary procedure) katika Mahakama yenye mamlaka ya kusikiliza shauri hilo.





Makosa na adhabu

17. Mtu ye yote ikiwa ni mnunuzi, muuzaji, wakala au mkusanya kodi ambaye:-

(a) ameshindwa, amedharau au amekaidi kuwasilisha kodi chini ya Sheria Ndogo hizi;

(b) ameshindwa, amedharau au amekaidi kuwasilisha kodi aliyokusanya kwa Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hizi;

(c) ameshindwa au amekaidi kuleta taarifa zo zote ambazo zinahitajika kuthibitisha makusanyo yake kwa Halmashauri;

(d) atamshawishi mtu ye yote asilipe au atamzuia mkusanya kodi ye yote kufanya kazi yake;

(e) atadanganya, na katika kufanya hivyo akaikosesha Halmashauri mapato yake;

(f) atashindwa kuhifadhi kumbukumbu na mahesabu yanayohitajika chini ya Sheria Ndogo hizi.

atakuwa ametenda kosa chini ya Sheria Ndogo hizi na akithibitika kuwa na hatia ya kosa hilo atawajibika kulipa deni hilo na atawajibika kuilipa Halmashauri faini isiyopungua laki tatu (300,000/=) na ushuru aliotakiwa alipe au kifungo cha mwaka mmoja.

Hati ya kukamata mali na kuiuza kwa mnada mali ya mdaiwa

18.-(1) Bila ya kuathiri Sheria Ndogo ya 11, 12, 13 na 16, Halmashauri itakuwa na uwezo wa kisheria wa kuomba katika Mahakama yenye Mamlaka katika eneo la Halmashauri kwa kutumia Hati kukamata mali na kuiuza kwa mnada kwa kutumia hati iliyomo katika jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Hati atakayopewa mlipa kodi na Mahakama, itakuwa na mamlaka ya kisheria ya kukamata na kuuza mali inayoondosheka ya mlipa kodi na kila hati ya madai ambayo itapelekwa Mahakamani kwa njia ambayo imeelezwa katika Sheria Ndogo hii, itakuwa ni uthibitisho kamili wa maelezo ya madai yaliyoelezwa chini ya hati hiyo.

Sura ya 33 ya Sheria za Tanzania

19. Bila ya kuathiri maelekezo ya jumla ya Sheria Ndogo hi Halmashauri itatumia Sheria ya mwenendo wa mashauri ya madai (C provedure Act) katika kudai deni la kodi na Halmashauri itapata fi kutokana na deni hilo kwa kiasi cha fidia kinachotolewa na benki K kwa wakati husika.

---

JEDWALI

---

HALMASHAURI YA WILAYA YA KILINDI

HATI YA KUKAMATA MALI NA KUIUZA

*(Limetengenezwa chini ya Sheria Ndogo ya 21)*

JINA LA MALI:........................................................................................................

KWA DALALI WA MAHAKAMA

..................................................................

..................................................................

..................................................................

..................................................................

Hii ni kukuamuru kukamata na kuitunza mali inayoondosheka y .....................................ambayo imeonyeshwa katika Jedwali, mpaka hapo mtajwa hap juu atakapolipa shilingi......................................... zikiwa ni deni la ushuru analodaiw pamoja na riba kwa kiwango cha asilimia moja (1%) kwa kila mwezi, kuanzi tarehe.................... mwezi...............mwaka..........mpaka tarehe...............mwezi.......... mwaka...................Ikiwa ni pamoja na gharama za kukamata mali hiyo. Na baada y kutoa taarifa (notice) ya siku kumi na nne ambayo itabandikwa katika jengo la mahakam na baada ya kumalizika kwa taarifa hiyo, mauzo ya mali hiyo yataanza kwa mnada il kupata shilingi.................................. Pamoja na riba na gharama za kukamatia mali hiy

UNAAMRIWA kurudisha hati hii mnamo au kabla ya tarehe.................. mwezi..................Mwaka..................... Pamoja na maelezo ya namna ulivyotekele amri hiyo au sababu kwa nini kututekeleza (kama ndivyo).

Imetolewa na mimi na kugongwa mhuri wa Mahakama leo tarehe.........................mwez ...................... Mwaka.................

.........................................

HAKIMU





Muhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi umetiwa katika Sheria Ndogo hizi kufuatia mkutano wa Baraza la Madiwani ambalo uliitishwa na kufanyika katika Ukumbi wa Halmashauri tarehe 19 mwezi 9 mwaka 2007 mbele ya hawa wafuatao:

BIBI KUDRA J. MWINYIMVUA,
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi*

L.S.

MHE. SALIMU M. KIBONGE,
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya wilaya ya Kilindi*

NAKUBALI

Dodoma,
18 Mei, 2009

MHE MIZENGO KAYANZA PETER PINDA (MB.),
*Waziri Mkuu*

---

TANGAZO LA SERIKALI NA. 252 la tarehe 24/7/2009

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)
(SURA YA 287)

## SHERIA NDOGO

*Zimetungwa chini ya kifungu cha 153*

SHERIA NDOGO ZA (HIFADHI YA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA KILINDI, 2009

### SEHEMU YA KWANZA
UTANGULIZI

1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (Hifadhi ya Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi, 2009 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali. Jin tar mv ku

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika maeneo yote ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi. Ma

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo:- Taf

"Afisa mwidhinishwa" maana yake ni afisa maliasili, afisa kilimo na mifugo pamoja na afisa ye yote wa Halmashauri atakayeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;